# Maelezo muhimu kwa mwekezaji

**Hati hii inatoa taarifa muhimu kwa wawekezaji katika FCPE hii. Si hati ya uendelezaji. Taarifa iliyopo imetolewa kwako kwa mujibu wa wajibu wa kisheria ili kukuwezesha kuelewa ni nini hasa uwekezaji katika FCPE hii, na ni hatari gani zinazohusishwa. Unashauriwa kuisoma ili kufanya uamuzi sahihi ikiwa utawekeza au la.**

## MPANGO WA UMILIKI WA HISA KWA WAAJIRIWA WA L'OREAL

**Msimbo AMF: (C) 990000120159**

Hazina hii ya Uwekezaji wa Kampuni (FCPE) inasimamiwa na Amundi Asset Management, kampuni ya kundi la Amundi
FCPE- Hazina ya Akiba ya Waajiriwa kwa mujibu wa sheria ya Kifaransa

## Malengo na sera ya uwekezaji

Upambanuzi wa Autorité des Marchés Financiers: "imewekeza katika dhamana zilizoorodheshwa za Kampuni".
Kwa kujisajili katika MPANGO WA UMILIKI WA HISA KWA WAAJIRIWA WA L'OREAL, ("FCPE"), unawekeza katika hisa za L'OREAL.
Lengo la usimamizi wa FCPE ni kufuatilia utendaji wa hisa za L'OREAL, zinapopanda au kushuka.
Ili kufikia lengo hili, FCPE imewekeza angalau 95% katika hisa za L'OREAL na baki katika OPCVM na/au FIVG iliyowekwa kama "fedha" na/au "fedha za muda mfupi" na/au kwa fulusi.
Thamani halisi ya mali ya FCPE itapanda na kushuka, kulingana na ukadiriaji wa hisa ya L'OREAL, kwa mujibu wa asilimia ya mali iliyowekezwa katika hisa hizi.
Mapato na faida ya mtaji halisi yaliyokamilika kwa Hazina ni lazima yawekezwe tena.
Unaweza kukomboa vitengo vyako kila siku, na malipo ya kukomboa yanafanywa kila siku kama ulivyoelezwa katika kanuni za FCPE.
Kipindi cha uwekezaji kilichopendekezwa: Miaka 5.
Muda huu hauzingatii muda wa kuzuia akiba yako.

## Maelezo mafupi juu ya hatari na ufanisi

Kwa hatari ndogo, ← → Kwa hatari kubwa,

kuna uwezekano wa mazao madogo — kuna uwezekano wa mazao makubwa

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **6** | |

FCPE ina hatari ya hatua ya 6, ambayo ni kiwango cha kawaida katika ulimwengu wa uwekezaji.

Data ya kihistoria iliyotumiwa kuhesabu kiashiria cha nambari ya hatari, haiwezi kuwa ishara ya kuaminika katika kuelezea hatari ya baadaye ya FCPE.
Kategoria ya hatari inayohusishwa na FCPE hii si hakikisho na inaweza kubadilika.
Kategoria ya chini kabisa haimaanishi "kutokuwa na hatari".
Mtaji uliowekezwa awali hauna uhakikisho.

Hatari kuu za FCPE ambazo hazijazingatiwa katika kiashiria ni:

- Hatari ya fedha: katika hali fulani ambapo kiasi cha ubadilishaji kwenye masoko ya kifedha ni duni sana, ununuzi au uuzaji wowote kwenye masoko haya unaweza kusababisha mabadiliko makubwa ya soko.

Kuwepo kwa hatari zozote kama hizi kunaweza kuwa na athari mbaya kwenye thamani ya mali katika uwekezaji kwa ujumla.

## Ada

Ada na kodi zinazotozwa hutumiwa kugharamia uendeshaji wa FCPE ikiwa ni pamoja na gharama za usambazaji wa vitengo, ada hizi hupunguza uwezekano wa kukua kwa uwekezaji.

| Ada za wakati mmoja ambazo hutozwa kabla au baada ya uwekezaji | |
|---|---|
| **Ada ya kuingia** | Hakuna |
| **Ada ya kuondoka** | Hakuna |
| Kodi hizi zinahusiana na asilimia ya kiwango cha juu zaidi ambayo inaweza kuondolewa kutoka kwa mtaji wako kabla ya uwekezaji (kuingia) au ukomboaji (kutoka). Mwekezaji anaweza kupata viwango vya kuingia na kutoka vinavyohusiana naye, kutoka kwa kampuni yake na/au mmiliki wa akaunti yake,. | |
| Ada zinazotozwa na FCPE kwa mwaka mmoja | |
| **Gharama za uendeshaji** | 0.10% ya wastani wa mali halisi |
| Ada zinazotozwa na FCPE katika hali fulani | |
| **Malipo ya utendaji** | Hakuna |

Gharama **za uendeshaji** zinategemea takwimu za mwaka uliopita za fedha. Asilimia hii inaweza kubadilika kutoka mwaka mmoja hadi mwingine. Haijumuishi:

- ada za kati, isipokuwa ada za kuingia na kutoka zilizolipwa na FCPE wakati wa kununua au kuuza hisa za hazina nyingine ya pamoja

Kwa kuwa FCPE bado haijasimamisha akaunti zake, asilimia ya gharama za uendeshaji zilizotolewa kinyume ni makadirio.
Kwa kila mwaka wa fedha, ripoti ya mwaka ya FCPE itatoa kiasi halisi cha gharama zilizotumika.

Kwa habari zaidi kuhusu ada za FCPE hii, tafadhali angalia sehemu za "gharama" katika kanuni zake zinazopatikana kwenye tovuti ya www.amundi-ee.com.

## Utendaji wa awali

*FCPE yako bado haina data ya mwaka kamili wa kalenda inayoonyesha chati ya utendaji.*

FCPE imeidhinishwa.
Fedha ya rejeo ni yuro (EUR).

## Maelezo muhimu

Jina la mdhamini: Benki ya CACEIS.
Jina la mmiliki wa akaunti: Amundi Tenue de Comptes na/au, ikiwezekana, msimamizi mwingine yeyote aliyeteuliwa na Kampuni.
Fomu ya kisheria ya FCPE: kikundi kilichobinafsishwa.
Kulingana na mfumo wako wa kodi, faida yoyote ya mtaji na mapato kutoka kwa vitengo vya FCPE yanaweza kutozwa kodi.
Hazina hii haijafunguliwa kwa wakazi wa Marekani / "Mtu wa Marekani" (ufafanuzi unapatikana kwenye tovuti ya Kampuni ya usimamizi: www.amundi.com).
Bodi ya usimamizi inajumuisha wawakilishi 4 wa wanahisa na wawakilishi 3 wa kampuni iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika kanuni za FCPE. Kazi zake ni kupitia ripoti ya kila mwaka ya FCPE na taarifa za kifedha, usimamizi wa fedha, utawala na uhasibu. Hasa, hufanya uamuzi kuhusu kuunganisha, kutenganisha au shughuli za fedha. Kwa maelezo zaidi, tafadhali angalia kanuni.
Bodi ya usimamizi hujihusisha katika haki za kupiga kura zilizounganishwa na hisa za kampuni.

Taarifa ya mara kwa mara kuhusu kampuni inapatikana kwa ombi kutoka kwa kampuni.
Udhibiti na hati za hivi karibuni za taarifa za udhibiti wa FCPE, pamoja na maelezo mengine, yanapatikana bila malipo kutoka kwa kampuni ya usimamizi.

Thamani halisi ya mali inapatikana kwenye tovuti www.amundi-ee.com.
Amundi Asset Management inaweza kuwajibika tu kwa msingi wa taarifa yoyote iliyo katika hati hii ambayo inapotosha, isiyo sahihi au haiendani na sehemu husika za kanuni za FCPE.

---

FCPE hii imeidhinishwa nchini Ufaransa na inasimamiwa na Autorité des Marchés Financiers (AMF).
Kampuni ya usimamizi, Amundi Asset Management, imeidhinishwa nchini Ufaransa na inasimamiwa na Autorité des Marchés Financiers (AMF).
Habari hii muhimu ya mwekezaji ni sahihi na ya kisasa zaidi mnamo tarehe 1 Mei 2018.